**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

**WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE**

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE

**MHESHIMIWA MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM),**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA, KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**JUNI, 2024**

# YALIYOMO


YALIYOMO .................................................................................... i

VIFUPISHO.................................................................................... iv

A. UTANGULIZI.............................................................................. 1

B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA............................. 3

MUUNDO WA WIZARA.......................................................... 3

MAJUKUMU YA WIZARA..................................................... 4

C. MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 .................................................................................. 4

SEKTA YA UTALII ..................................................................... 4

SEKTA YA MAMBO YA KALE .................................................. 7

CHANGAMOTO ZA WIZARA..................................................... 9

a. Mapato yaliyokusanywa na Wizara kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024) ....................................11

Fedha iliyopatikana kwa kipindi miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024)...................................................................12

D. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE ..............................................................13

Programu Kuu za Wizara ni : - ...................................................13

Programu ndogo za Wizara ni: - ................................................13

E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 .............................................14

F. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2023-MACHI 2024...............................................................16

I. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.

UTEKELEZAJI HALISI ............................................................17
II. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII....24
UTEKELEZAJI HALISI ............................................................24
III. PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII..........................................................................28
UTEKELEZAJI HALISI ............................................................29
IV. KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII .31
UTEKELEZAJI HALISI ............................................................31
UTEKELEZAJI HALISI ............................................................33
V. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE .........................35
UTEKELEZAJI HALISI ............................................................35
UTEKELEZAJI HALISI ............................................................38
UTEKELEZAJI HALISI ............................................................40
G. VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025. ..42
H. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ...........................................................................43
I. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU . (PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ..............................................................44
Programu ya kwanza: Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe ....................................................45
Programu ya Pili: Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii ..........................................................46
Programu ya Tatu: Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii ..........................................................48

Programu ya Nne: Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii ....................................................49
Programu ya Tano: Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale............................51
J. SHUKURANI ....................................................................................55
K. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ..........................................................................................60
L. HITIMISHO .......................................................................................61
VIAMBATISHO .....................................................................................62
Kiambatisho Namba1A.............................................................................62
Kiambatisho Namba1B.............................................................................64
Kiambatisho Namba1C.............................................................................65
Kiambatisho Namba1D.............................................................................66
Kiambatisho Namba1E.............................................................................68
Kiambatisho Namba1F ............................................................................70
Kiambatisho Namba1G.............................................................................72
KIAMBATISHO 2 ................................................................................ 73

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BASSFU | Baraza la Sanaa Sensa ya filamu na Utamaduni |
| BLM | Baraza la Mapinduzi |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CNN | Cable News Network |
| DKT | Daktari |
| FM | Frequency Modulation |
| GIS | Geographic information system |
| HAZ | Hotel Association Zanzibar |
| IAA | Institute of Accountancy Arusha |
| IDA | International Development Association |
| IORA | Indian Ocean Rim Association |
| ITB | International Tourism Borse |
| JUHIMKO | Jumuia ya Hifadhi Mji Mkongwe |
| MBM | Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi |
| MICE | Meetings Incentives Conferences and Exhibitions |
| MoU | Memorandum of Understand |
| NMB | National Microfinance Bank Limited |
| PATI | Pemba Tourism Investors |
| PBB | Program Based Budget |
| PBZ | People Bank of Zanzibar |
| PDB | Presidential Delivery Bureau |
| SADEC | Southern Africa Development Community |
| SMT | Serikali ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SUZA | State university of Zanzibar |
| TATO | Tanzania Association of Tour operators |
| TBC | Tanzania Broadcasting Cooperation |

| | |
|---|---|
| TBC | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| TBI | Tone Blair institute |
| UNDP | United Nation Development Programme |
| UNECA | United Nations Economic Commission for Africa |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| UNICEF | United Nations Children's Fund |
| UNWTO | United Nation World Tourism Organization |
| USAID | United States Agency for International Development |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZATI | Zanzibar Association for Tourism Investor |
| ZATO | Zanzibar Association for tourism Operator |
| ZATOGA | Zanzibar Tour Guide Association |
| ZAWA | Zanzibar Water Authority |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Cooperation |
| ZCTV | Zanzibar Cable Television |
| ZECO | Zanzibar Electricity Cooperation |
| ZIPA | Zanzibar Investimate and Promotion Authority |
| ZSSF | Zanzibar Social Security Fund |

# HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE, MHESHIMIWA MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA, KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025, AKIWASILISHA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu muweza wa kila kitu, kwa kuendelea kutupa neema ya uhai na uzima pamoja na kutujaalia kuweza kukutana leo hii, katika vikao hivi vya kujadili Makadirio na Matumizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Makadirio hayo yanalenga kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara kwa maslahi mapana ya wananchi wa Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema katika kutekeleza jukumu hili pamoja na kutupa hekima, busara na uaminifu wakati wa kutekeleza majumu yetu ya kila siku.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwa udhati kabisa, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuleta Mapinduzi ya Maendeleo ambayo yanachangia kukuza Uchumi wa nchi. Harakati hizi za Maendeleo zimekuwa zikiendelea kwa kasi katika maeneo mengi ya Mjini na Vijijini, ambapo sote tumekuwa mashahidi wa kujionea kazi hizo za maendeleo. Aidha, niendelee kumpongeza kwa kuitekeleza kwa vitendo Ilani

ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 - 2025, ambayo inalenga kuleta mageuzi makubwa katika nchi yetu, ni imani yetu kwamba kutokana na kasi ya maendeleo inavyokwenda basi tayari malengo mengi na ahadi za Ilani ya CCM zimeshavukwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Mheshimiwa Rais wetu afya njema pamoja na kumzidishia Hekima, Maarifa na Uadilifu wakati akiendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar pamoja na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kuchapa kazi kwa kiwango cha hali ya juu na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya nchi pamoja na kuendelea kuibakisha nchi yetu katika hali ya Umoja, Upendo na Mshikamano huku tukijivunia Amani na Utulivu uliotawala unaotuletea maendeleo ya kasi.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii adhimu, kukupongeza wewe Spika wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wasaidizi wako wote akiwemo Naibu Spika, Wenyekiti wa Baraza, Katibu wa Baraza, Wenyeviti wa Kamati, Wajumbe wa Baraza, Maofisa na Wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa jitihada za hali ya juu wanazozitumia katika kufanikisha majukumu ya Baraza hili.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii, kuishukuru Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa

Malengo na Majukumu tuliyojipangia pamoja na kutupa miongozo na maelekezo ya namna ya kufikia malengo ya Wizara. Pia, niwapongeze Makatibu wote wa Kamati hii kwa kuratibu shughuli za Kamati kwa ufanisi wa hali ya juu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie upendo baina yetu na atuwezeshe kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya Taifa.

## B. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

6. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imeundwa kwa lengo la kusimamia Sekta Kuu mbili ambazo ni Utalii na Mambo ya Kale. Vile vile, Wizara hii imepewa majukumu ambayo huyatumia katika kupanga malengo ya Idara na Taasisi zetu.

## MUUNDO WA WIZARA

7. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inasimamia Taasisi na Idara zifuatazo : -

   i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi

   ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

   iii. Idara ya Utalii

   iv. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale

   v. Kamisheni ya Utalii Zanzibar

   vi. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe

   vii. Ofisi Kuu Pemba

**MAJUKUMU YA WIZARA**

**8. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine pia inatekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

ii. Kukuza pato la nchi kupitia Sekta ya Utalii.

iii. Kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha miradi ya utalii itakayotoa tija kwa wananchi.

iv. Kuyalinda, kuyahifadhi na kuyatangaza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini.

v. Kuvitunza vitu na mabaki ya kihistoria yaliyopo nchini ili kuweka kumbukumbu kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

vi. Kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar.

## C. MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**9. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengine imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:

**SEKTA YA UTALII**

i. Wizara imefanikiwa kupokea ujumbe wa watu 150 kutoka nchini China, ujumbe huo umejumuisha msanii mashuhuri Bw. Jin Dong, madaktari na wasanii wengine. Aidha, msanii huyo alitayarisha filamu (Presidential

Tour) ambayo Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameshiriki katika utayarishaji wake katika eneo la Mnemba na Mji Mkongwe. Filamu hiyo itaoneshwa katika televisheni za China na nchi jirani, hali hiyo itapelekea utalii wa Zanzibar kutangazwa zaidi katika safu za kimataifa na kwa gharama nafuu zaidi.

ii. Wizara imepokea meli nane za kitalii kwa upande wa Pemba na Unguja ambazo ni MS Zuiderdam, MS Bolette Cruise Ship, Swan Hellenic, Silver Spirit, Norwegian Dawn Cruise Line, MS Poesia, Holland America Line Zuiderma Voyage, National Geographic Explorer na MS World ambayo ni meli kubwa duniani yenye makazi binafsi ikiwa na vyumba vikubwa 165 vinavyoweza kununuliwa kwa kwa Dola Million 4 za Kimarekani kwa kila kimoja. Aidha, meli hizo zimeleta jumla ya watalii 8,649 ambao wamepata fursa ya kuvitembelea vivutio vya utalii vilivyopo nchini. Kuja kwa meli hizo zinachangia kukua kwa utalii wa meli ambao huleta tija kubwa kwa sekta ya utalii.

iii. Wizara imeandaa Tamasha la Utalii na Utamaduni (Pemba Tourisport Bonanza and Culture) lilojumuisha michezo ya kiutamaduni inayofanyika sana kwa Pemba ikiwemo mchezo wa ng’ombe, resi za ngalawa, mashindano ya dufu, paredi ya punda, ngoma za asili, kuogelea, “Triathlon” (kuogelea, kupanda baiskeli na kukimbia) na “Duathlon” (kukimbia na kupanda baiskeli). Aidha, Tamasha hili limehudhuriwa na mtangazaji maarufu aitwae Richard Quest kutoka kituo cha televisheni cha CNN ya nchini Marekani, ambapo

inakisiwa kituo hicho kinawafikia zaidi ya watu bilioni mbili kutoka mataifa mbali mbali duniani. Kufanyika kwa shughuli hizo kwa upande wa Pemba kunalenga kukifungua kisiwa hicho kiutalii.

iv. Kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini mwaka 2023 kwa asilimia 16.4 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022 hadi kufikia watalii 638,498 mwaka 2023, ongezeko hili linatokana na kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya awamu ya nane katika uimarishaji wa miundombinu ya kimkakati, huduma bora, mazingira mazuri ya sekta binafsi. Pamoja na Wizara kuitangaza nchi kupitia ushiriki katika mikutano ya kimataifa, ubunifu katika utangazaji wa rasilimali na vivutio vyetu, maonesho pamoja na matamasha mbali mbali ya utalii.

v. Wizara  kupitia Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kushiriki katika maonesho saba ya kitaifa na manne ya kimataifa ambayo yamevitangaza vivutio vya utalii pamoja na kuhamasisha utalii hapa nchini, maonesho hayo ni nane nane – Kizimbani, Kizimkazi Festival - Paje, "Holiday Market Festival" - Maisara, Fahari ya 8 Mzanzibari – Golden Tulip, Kilimo Hai – Kizimbani, Sabasaba - Dar es salaam na "Swahili International Expo" (SITE) - Dar – es - Salaam. Aidha, Kamisheni ya Utalii imeshiriki katika maonesho ya wazi ya "My Tanzania Roadshows" yaliyofanyika katika miji ya Geneva (Switzerland), Lyon (Ufaransa) na Milan (Italy), maonesho ya Biashara mjini Berlin– Ujerumani. Pia, Kamisheni imeshiriki kwenye uzinduzi wa safari za ndege za moja kwa moja kutoka Lisbon Ureno hadi Zanzibar kupitia Shirika la ndege la Hifly pamoja

na kufanya ziara nchini Korea ya Kusini kutafuta wawekezaji wa kuwekeza katika utalii wa mikutano (MICE Tourism).

vi. Wizara imeandaa Mradi wa uwezeshaji wa jamii wa kuboresha Mashamba ya Viungo ndani ya dhana ya utalii. Mradi huo unalenga kuimarisha baadhi ya mashamba ya viungo yaliyopo Unguja na Pemba kwa kuwapa wakulima mafunzo ya kilimo na utalii jumuishi, na kuweka huduma bora za kuwavutia watalii katika mashamba hayo ya viungo. Kwa hatua ya awali jumla ya mashamba 20 yatapandishwa miti ya viungo kwa kusimamiwa kwa pamoja baina ya wataalamu wa Kilimo na Utalii. Mradi huo unafadhiliwa na Taasisi ya World Vegetable Centre ambao unagharimu Dola za Kimarekani 85,000 kwa awamu ya mwanzo.

## SEKTA YA MAMBO YA KALE

i. Wizara imesaini hati tatu za Makubaliano (MoU) na taasisi mbali mbali za kitaifa na kimataifa. Taasisi hizo ni pamoja na Taasisi ya Makumbusho ya Taifa ya Tanzania, Chuo Kikuu cha York kutoka nchini Uingereza, Mfuko wa Prussian Heritage Fund kutoka nchini Ujerumani na Taasisi ya Makumbusho ya Oman. Mashirikiano hayo yanalenga kubadilishana uzoefu kwenye sekta ya Makumbusho na Mambo ya Kale ili kuifanya sekta hii kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia duniani.

ii. Wizara imefanikiwa kuweka jiwe la msingi katika eneo la Kihistoria la Mangapwani, shughuli hiyo ya uwekaji

wa jiwe la msingi ilikwenda sambamba na shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Eneo hilo la Mangapwani linaimarishwa kwa lengo la kurudisha uasili wake pamoja na kulinda na kuhifadhi historia kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

iii. Katika kutekeleza dhana ya uwekezaji katika maeneo ya kihistoria, Wizara imeingia mkataba na wawekezaji katika maeneo ya kihistoria ya Fukuchani kupitia kampuni ya YMH Limited, Zanzibar, Kisiwa cha Changuu (Changuu Lodge). Lengo la hatua hii ya uwekezaji ni kuongeza mapato kwa Serikali pamoja na kuyaweka maeneo hayo kuwa katika muonekano ulio bora. Aidha, Wizara imetangaza fursa za uwekezaji katika maeneo ya Kihistoria saba Unguja na Pemba na inaendelea kupokea maombi ya Wawekezaji. Maeneo hayo ni Kasri ya Maruhubi, Kasri ya Mtoni, Mkamandume, Pango la Kuumbi, eneo la kihistoria la Bi Khole, Mwinyi Mkuu Dunga, Chwaka Tumbe na eneo la kihistoria Mangapwani.

iv. Wizara kupitia Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe inaendelea na kazi ya kusimamia ujenzi wa Maegesho ya vyombo vya moto katika Eneo la Malindi. Mradi huu unatekelezwa kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na umefikia asilimia 80 ya utekelezaji. Kwa sasa wajenzi wanaendelea na kazi za uwekaji wa miundombinu ya maji, umeme na kupiga plasta. Kukamilika kwa mradi huu katika eneo la Mji Mkongwe kutaondoa adha kubwa ya uegeshaji wa vyombo vya moto bila ya mpangilio maalumu pamoja na kuondoa msongamano wa vyombo hivyo ndani ya Mji Mkongwe.

v. Wizara kupitia Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe imesimamia kazi za matengenezo makubwa ya Makaburi ya Wafalme yaliyopo pembezoni mwa Kasri la Wananchi la Forodhani, ujenzi wa makaburi hayo umefadhiliwa na Serikali ya Ufalme wa Oman. Tayari kazi hiyo imekamilika na yamefunguliwa rasmi mnamo tarehe 06/03/2024 na kuwashirikisha viongozi mbali mbali wa taasisi za Serikali pamoja na Ofisi ya Ubalozi Mdogo wa Oman. Kukamilika kwa matengenezo hayo pamoja na kuandikwa historia yake kumeongeza idadi ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini na kupelekea kuongezeka kwa siku za ukaazi wa wageni na kukuza pato la nchi.

vi. Wizara imekamilisha matayarisho ya Sera mpya ya Taifa ya Makumbusho na Urithi wa Mambo ya Kale ya mwaka 2023 ambayo kwa sasa ipo katika hatua za kuzinduliwa rasmi. Kuwepo kwa sera hii kutasaidia katika Kuyalinda, Kuyahifadhi pamoja na Kuyaendeleza maeneo na vitu vya kihistoria na mambo ya kale vilivyopo nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

## CHANGAMOTO ZA WIZARA

**10. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale licha ya kufanikiwa katika utekelezaji wa malengo na shughuli zake ilizojipangia, pia, inakabiliwa na changamoto mbali mbali miongoni mwao ni kama zifuatazo: -

i. Ushindani wa biashara ya utalii kutoka nchi zenye bidhaa zinazofanana na Zanzibar. Kama inavyofahamika kwamba utalii ni biashara kubwa duniani ambapo mataifa

hushinda katika utoaji wa huduma bora kwa lengo la kuwavutia wageni. Nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na changamoto hiyo kutoka kwa visiwa vyenye mfanano na Zanzibar kama visiwa vya Maldives, Mauritius, Seychelles na Reunion. Licha ya uwepo wa changamoto hiyo Wizara inaendelea na hatua za kuimarisha na kukuza huduma kwa wageni wanaoingia nchini ili waweze kuvutiwa zaidi.

ii. Uhaba wa fedha ambao huchangia kuikosesha Zanzibar kutangazwa katika masoko ya kimataifa. "Biashara itangazwayo ndio itokayo" kutokuwepo kwa matangazo katika masoko ya kimataifa kunaifanya Zanzibar kushindwa kutambulika vyema duniani na kupelekea kuleta idadi ndogo ya wageni wenye hadhi ya juu. Hali hii husababisha kupungua kwa mapato ya nchi pamoja na kutowafaidisha moja kwa moja wananchi kupitia sekta ya utalii. Licha ya uwepo wa changamoto hii Wizara inashirikiana na wadau wa utalii katika kuyafikia masoko zaidi ya kimataifa ya hadhi ya juu ili kuweza kupata idadi kubwa ya wageni watakaoweza kuingia nchini.

iii. Uvamizi katika maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini. Kwa kipindi kirefu maeneo mengi ya kihistoria yaliyopo nchini yalikosa ushughulikiaji wa karibu, hali ilyopelekea wananchi waliopo karibu na maeneo hayo kuyavamia kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makaazi. Kadhia hii imepelekea kuharibika kwa kasi kwa maeneo hayo pamoja na kupoteza uhalisia na historia ya sehemu husika. Kuwepo kwa changamoto hiyo Wizara inachukua jitihada za makusudi ya kuyapima na kuyahifadhi maeneo hayo ya kihistoria.

iv. Ukiukwaji wa masharti ya vibali kwa wamiliki wa nyumba za Mji Mkongwe ambao huyafanyia matengenezo majengo yao kinyume na vibali walivyoomba. Hali hii hupelekea kupoteza uhalisia wa majengo yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe imekuwa ikichukua jitihada kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha ukarabati unafanyika kwa mujibu wa vibali vinavyotolewa pamoja na kuwaelimisha wakaazi na wadau wa Mji Mkongwe juu ya faida zinazopatikana katika kuuhifadhi na kuuendeleza mji huu wa kihistoria.

v. Ukiukwaji wa masharti ya Uwekezaji wa Mahoteli ya Kitalii ikiwemo kutofuata sheria za mazingira na ujenzi. Baadhi ya wawekezaji wa mahoteli katika maeneo maarufu ya kitalii kisiwani Unguja wamekuwa wakikiuka masharti na sheria za uwekezaji pamoja na kutofuata kanuni za mipango miji katika maeneo hayo. Hali ambayo ni hatarishi wakati yanapotokezea maafa kama janga la moto, jambo ambalo linaleta ugumu wakati wa uokozi wa watu na mali zao. Kutokana na changamoto hii, Wizara ipo katika mchakato wa ukamilishaji wa Waraka wa jambo hilo ili uwasilishwe Serikalini kwa lengo la kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

**a. Mapato yaliyokusanywa na Wizara kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024)**

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale katika mwaka wa fedha 2023/2024 imepangiwa kukusanya **Shilingi 1,000,000,000/=** na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kukusanya **Shilingi 775,068,586/=** sawa na

**asilimia 77.5.** Fedha zote zimeingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, kupitia Kamisheni ya Utalii ambayo mapato yake hutumia kwa ajili ya shughuli za utangazaji utalii pamoja na uendeshaji wa ofisi imepanga kukusanya **Shilingi 10,295,888,120/=** na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kukusanya **Shilingi 6,266,227,895.5/=** sawa na **asilimia 61**, Kati ya hizo **Shilingi 2,200,000,000/=** zimeingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina. (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1B**).

b. **Fedha iliyopatikana kwa kipindi miezi tisa (Julai 2023-Machi 2024)**

12. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale iliidhinishiwa matumizi na Baraza la Wawakilishi ya **Shilingi 13,984,900,000/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tatu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Kati ya hizo **Shilingi 2,858,000,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 4,126,900,000/=** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 7,000,000,000/=** kwa kazi za Maendeleo. Aidha, Kamisheni ya Utalii iliidhinishiwa makusanyo ya matumizi ya **Shilingi 10,295,888,120/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu mbili, kati ya hizo **Shilingi 1,725,888,120/=** Kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 3,770,000,000/=** kwa ajili ya kazi za kawaida na **Shilingi 4,800,000,000/=** zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

13. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2024, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilipata jumla ya **Shilingi 5,801,762,489/=** sawa na **asilimia 41.47**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 976,522,746/=** zilipatikana kwa kazi za

kawaida sawa na **asilimia 34**. **Shilingi 3,210,585,372/=** zilipatikana kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 77.8**, na kwa ajili ya utekelezaji wa miradi sawa na **asilimia 23.** Aidha, Kamisheni ya Utalii ilifanikiwa kupata **Shilingi 1,221,515,480/=** kwa ajili ya mishahara, sawa na **asilimia 71** na **Shilingi 1,440,219,994/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na **asilimia 38**. (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1A**).

## D. PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza Malengo na Majukumu kwa kufuata Mfumo Maalumu wa Bajeti (Program Based Budget, PBB), ambapo Wizara inasimamia programu kuu tano na programu ndogo tatu.

**Programu Kuu za Wizara ni : -**

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.

ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.

iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

**Programu ndogo za Wizara ni: -**

i. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.

ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

## E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**15.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kutekeleza 'Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Maeneo ya Kihistoria' kwa kuyafanyia matengenezo maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu – Pemba

ii. Kuimarisha eneo la kihistoria la Mangapwani – Unguja

iii. Kuimarisha Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni – Unguja na

iv. Kuimarisha eneo la Kihistoria la Maruhubi – Unguja

**16.** **Mheshimiwa Spika,**

***Eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu – Pemba***

Mradi wa kuimarisha eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba unatekelezwa na Kampuni ya Yassin & Sons LTD, ambapo mradi huu umeanza kutekelezwa Mei mwaka 2023 na ulitarajiwa kukamilika baada ya mwaka mmoja. Mradi huu umegharimu **Shilingi 2,407,316,675/=** na hadi kufikia Machi 2024 mjenzi amelipwa **Shilingi 479,663,920.5/=.** Utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 40** ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa majengo ya

maduka, ofisi na mkahawa. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na uwezekaji wa majengo mapya, kufikisha umeme katika eneo la mradi, uondoshaji wa fusi katika majengo ya kale ya kihistoria pamoja na kuziba nyufa za majengo hayo.

17. **Mheshimiwa Spika,**

***Eneo la Kihistoria la Mangapwani – Unguja***

Mradi wa kuimarisha eneo la kihistoria la Mangapwani Unguja unatekelezwa na Al Hilal Company LTD, ambapo mradi huu umeanza kutekelezwa mwaka 2023 na unatarajiwa kukamilika Juni 2024 mradi huu umegharimu **Shilingi 2,238,544,230/=** na hadi kufikia Machi 2024 mjenzi amelipwa **Shilingi 770,319,366/=.** Utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 85**. Pia utekelezaji wa mradi huu unahusisha maeneo makuu matatu ya kihistoria ambayo ni Kisima cha chini kwa chini, mabaki ya mahandaki ya vita vya pili vya Dunia pamoja na Handaki la kuhifadhia watumwa. Kazi zilizofanyika katika maeneo hayo ni pamoja na ujenzi wa majengo ya maduka, ofisi na mkahawa. Ukarabati wa ngazi za kushukia katika kisima cha chini kwa chini, ukarabati wa mahandaki ya vita vikuu vya pili vya Dunia, ukarabati wa handaki lililotumika kuhifadhia watumwa pamoja na ujenzi wa ukuta kwa ajili ya kuyalinda na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria yaliyopo katika eneo hilo.

18. **Mheshimiwa Spika,** mradi wa Kuimarisha Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni pamoja na mradi wa Kuimarisha eneo la Kihistoria la Maruhubi – Unguja ipo katika hatua za manunuzi. Mradi wa eneo la

Kihistoria la Maruhubi kwa sasa timu ya kufanya tathmini ya kupata mjenzi imeanza kazi ili kumpata mjenzi wa mradi huo. Aidha, kwa upande wa Kuimarisha Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni upo katika hatua za kuandaa michoro ambapo mradi huu utatekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

19. **Mheshimiwa Spika,** kuendelea kuyaimarisha maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini ni kuendeleza lengo la kuyalinda, kuyahifadhi na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho. Aidha, kazi hizo za uimarishaji wa maeneo ya kihistoria kunapelekea kuongezeka kwa idadi ya vivutio vya watalii vilivyopo nchini, ambavyo vinachochea ongezeko la mapato ya nchi pamoja na ongezeko la siku za ukaazi kwa wageni wanaoingia nchini.

## F. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI 2023-MACHI 2024.

20. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipanga kutekeleza programu kuu tano kama ifuatavyo: -

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.

ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii.

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.

iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii.

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale

**I. PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE.**

**21. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya eneo la urithi la Mji Mkongwe na maeneo ya kihistoria yaliyohifadhiwa, kuimarishwa na kuendelezwa kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Matokeo ya muda mrefu ni kuyahifadhi, kuyalinda, kuyatangaza na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini pamoja na Uhifadhi wa Mji Mkongwe ili kubakia kuwa urithi wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

**22. Mheshimiwa Spika,** programu hii ya Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe inatekelezwa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe.

**23. Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa na programu hii ni Uhifadhi na Uendelezaji wa Makumbusho, Maeneo ya Kihistoria, Mambo ya Kale pamoja na Mji Mkongwe.

**UTEKELEZAJI HALISI**

**24. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Arkansas nchini Marekani wamefanya tafiti za akiolojia katika maeneo ya Dunga, Kizimbani, Machui, Kombeni, Maungani, Jumbi, Kama, Bububu na Mwakaje. Tafiti hizo zimelenga kuyatambua maeneo mapya ya kihistoria

ambayo hayajawahi kufanyiwa tafiti zozote, katika tafiti hizo kumepatikana baadhi ya mabaki ya vyungu na vyuma ambavyo vinathibitisha uwepo wa makaazi ya watu kwenye karne zilizopita katika maeneo hayo.

25. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za uimarishaji wa Makumbusho yaliyopo nchini, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imeanzisha Makumbusho mpya ya Sanaa iliyopo Mnazi Mmoja. Makumbusho haya yanalenga kutunza kumbukumbu ya Wanyama na Viumbe Hai waliopo nchini. Miongoni mwa wanyama waliopo katika makumbusho hayo ni pamoja na Makobe, vipepeo na aina mbali mbali za ndege. Kuwepo kwa makumbusho haya kunaongeza idadi ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini na kutunza historia kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

26. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuyalinda na kepusha uvamizi katika maeneo ya kihistoria, Hati Miliki mbili za maeneo ya kihistoria ya Bi Khole na Mwera zimepatikana. Kupatikana kwa Hati Miliki za maeneo hayo kutasaidia kulinda na kuhifadhi historia za sehemu hizo. Aidha, Idara inaendelea na taratibu za kupata Hati Miliki nyengine mbili za maeneo ya Mtoni na Kijichi. Vile vile, ukaguzi wa maeneo 10 ya kihistoria yaliyopo Pemba umefanyika kwa ajili ya kuanza taratibu za kuyapima na hatimae kuyapatia Hati Miliki maeneo hayo. Maeneo yenyewe ni Ras Mkumbuu, Mkamandume, Jambangome, Ngome Kongwe, Fufuni, Kichokochwe, Ole Mandani, Chwaka Tumbe, Pango la Kijiji na Msuka Mjini.

27. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeendelea na kufanya matengenezo mbali mbali madogo madogo ya meneo ya kihistoria kisiwani Pemba ikiwemo uwekaji wa mabango mbali mbali ya maelezo kuhusiana na maeneo hayo ya kihistoria ikiwemo eneo la Kihistoria la Chwaka – Tumbe, Mkamandume na Jambangome pamoja na kufanya matengenezo ya kaburi la kihistoria la Sharif katika eneo la msitu wa Ngezi. Pia, Idara inaendelea na mchakato wa ulipaji fidia kwa wanajamii wanaozunguka maeneo ya kihistoria kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa. Kadhalika, Idara imefanya matengenezo katika eneo la kihistoria la Kasri la Mtoni, ambalo liliathirika kutokana na mvua kubwa zilizonyesha hivi karibuni.

28. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imetayarisha rasimu ya Sheria ya kuanzishwa kwa Taasisi itakayoupa nguvu muundo wa hivi sasa unaoshughulikia usimamizi na uhifadhi wa Makumbusho na Mambo ya Kale. Kwa sasa, rasimu hiyo ipo katika utaratibu wa mapitio ya kisheria kabla ya kuwasilishwa katika Baraza lako Tukufu.

29. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeandaa Makala mbili, moja inaonesha varanda za mbao (balcony) zilizomo katika eneo la Mji Mkongwe ili kudhibiti kupotea kwa veranda hizo za kihistoria. Makala nyengine inaonesha utafiti wa Akiolojia uliofanyika katika eneo la Ngome Kongwe mwaka 2022, utafiti huo uligundua mabaki ya vitu vya Kihistoria yakiwemo Makaburi, misingi ya Kanisa pamoja na vifaa vya matumizi ya nyumbani. Utafiti huo ulifanywa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Royal Agriculture kilichopo Uingereza.

30. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kukuza na kuendeleza ubora wa wafanyakazi Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imewajengea uwezo wafanyakazi wa kitengo cha Mambo ya Kale wa Unguja na Pemba kwa kuwapatia mafunzo kuhusiana na kanuni za uchambuzi wa mabaki ya Akiolojia. Aidha, Idara imewapatia mafunzo ya GIS (Geographic Information System) kwa lengo la kuenda sambamba na hali ya uhitaji duniani.

31. **Mheshimiwa Spika,** Idara imepokea jumla ya wageni 7,245 ambao wametembelea maeneo ya kihistoria yaliyopo Unguja. Kati ya hao wenyeji ni 432, wageni 899, wageni maalumu 26 na wanafunzi 5,888. Aidha kwa upande wa Pemba jumla ya wageni 1,655 wametembelea maeneo ya kihistoria kati ya hao 72 wageni, 248 wenyeji na 1,335 wanafunzi.

32. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kutoa elimu kwa jamii juu ya huduma na kazi zinazofanywa na Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, imeshiriki katika maonesho ya saba saba yaliyofanyika Mlimani City jijini Dar es Salaam, maonesho ya (Z-Summit) kwenye Mkutano wa Jumuiya ya Madola uliofanyika Zanzibar pamoja na maonesho ya biashara ya kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika Nyamanzi Zanzibar. Aidha, Idara imeandaa na kurusha hewani kupitia vyombo vya habari jumla ya vipindi 35, vipindi 29 kupitia Furaha FM Radio, kipindi kimoja ZBC Redio na vipindi vitano Idhaa ya Uturuki.

33. **Mheshimiwa Spika,** Idara imegharamia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi 11 kwa fani na ngazi tofauti. Wafanayakazi wanne katika fani

ya Uhusiano wa Umma ngazi ya Diploma, wafanyakazi wawili fani ya Utunzaji wa Kumbukumbu mmoja katika ngazi ya Shahada ya kwanza na mwengine ngazi ya Diploma, Pia wafanyakazi watano wamepatiwa mafunzo mafupi ya Ukutubi katika Chuo cha Taifa (SUZA). Aidha, Idara imewezesha upatikanaji wa vitendea kazi vya Ofisi vikiwemo vifaa vya kuandikia, vifaa vya usafi pamoja na kulipia huduma za maji, umeme na mafuta. Vile vile, Idara imegharamia safari za kikazi kwa watendaji kati ya Unguja, Pemba na Dar es Salaam kwa lengo la kufanikisha utendaji.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuweka muonekano mzuri na wenye kuvutia katika maeneo ya Mji Mkongwe, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe imefanya matengenezo ya bwawa la chemchem (fontain) liliopo katika bustani ya Forodhani na kulirudisha kwenye uasili wake. Hivyo kurudishwa kwa "Fountain" hiyo kumeleta haiba ya aina yake kwenye bustani hiyo ambapo wageni na wenyeji hutumia sehemu hiyo kwa ajili ya uchukuaji wa picha. Aidha, Mamlaka imefanya matengenezo ya vyoo vilivyomo ndani ya bustani hiyo na kuviweka katika muonekano mzuri ambapo vimegawika katika makundi ya wanawake, wanaume na watu wenye mahitaji maalumu. Pia, imefanya kazi ya uwekaji wa vigae (pavements) katika njia ambazo zipo katika hali mbaya, miongoni mwa njia zilizofanyiwa matengenezo ni pamoja na njia za Shangani, Mizingani na Forodhani. Vile vile, Mamlaka kwa kushirikiana na Kampuni ya "Infinity Development Co LTD" imefanya ukarabati mkubwa wa bustani ya Tenga na kwa sasa upo katika hatua za mwisho za kupanda miti.

35. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wa Mji Mkongwe imefanya maadhimisho ya Siku ya Mji Mkongwe kwa mwaka 2023 ambayo hufanyika kila ifakapo tarehe 02 Disemba ya kila mwaka. Kauli Mbiu ya mwaka huu ilikuwa 'Mji Safi na Salama Tushirikiane'. Maadhimisho hayo hufanyika kwa lengo la kutambua thamani ya Kipekee ya Mji Mkongwe Kitaifa na Kimataifa pamoja na kuelimisha jamii juu ya uhifadhi na usimamizi wa Mji Mkongwe. Maadhimisho hayo yamehudhuriwa na Jumuiya mbali mbali za Uhifadhi za ndani pamoja na kuwepo kwa maonesho yenye kutoa elimu juu ya uhifadhi wa majengo ya Mji Mkongwe.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika suala la utoaji elimu kwa wananchi na kuhakikisha kwamba wanapata elimu ya uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe, Mamlaka imekutana na wafanyabiashara waliovamia na kufanya biashara katika chochoro za mji Mkongwe na kuwataka kuondoka sehemu hizo kwa lengo la kuuhifadhi Mji Mkongwe. Aidha, Mamlaka imetoa elimu Skuli kumi za Msingi na Sekondari zilizomo ndani ya Mji Mkongwe zikiwemo Skuli ya Msingi Kajificheni, Skuli ya Msigi Mkunazi na Skuli ya Sekondari ya Hamamni elimu hiyo imehusiana na uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe.

37. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka inaendelea na kazi ya usimamizi wa Ukarabati wa Jengo la Beit el Ajaib ambapo Mkandarasi ameanza kazi ya kulihami jengo kwa kuweka vizuizi "Temporary Scaffolding" kwa ajili ya kuzuia dari kuanguka, kufanya "Literal and Internal Support" ili kupata uwezo wa kuondoa mabati na mirunda ya mbele kwa ajili

ya kuanza ujenzi wa sehemu iliyovunjika. Pia, Mamlaka inaendelea kusimamia kazi za Ukarabati wa Jengo la Kasri la Wananchi Forodhani ambapo hadi sasa imepitia na kutolea maoni ripoti za hali ya jengo, “concept design” na “Preliminary design” zilizowasilishwa na mshauri elekezi. Aidha, Mamlaka inapitia ripoti ya mwisho pamoja na “tender documents” zilizowasilishwa na Mshauri elekezi. Mshauri elekezi wa mradi huu ni kampuni ya “GMP Consulting Engineering”. Ikumbukwe kwamba miradi yote inafadhiliwa na Serikali ya Ufalme wa Oman na mradi wa ujenzi wa Beit el Ajaib unagharimu Dola za Kimarekani 21 Milioni.

38. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imegharamia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wanne, wawili ambao walipata mafunzo ya kuwajengea uwezo Watumishi wanaotarajia kustaafu yaliyofanyika Dar-es- Salaam, mmoja mafunzo ya wahasibu ya “CPD hours” na mmoja mafunzo ya Udereva kwa wafanyakazi wa SMZ. Aidha, Mamlaka imelipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi watatu na stahiki za malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi tisa.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 10,085,599,000/=** na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **Shilingi 2,926,978,743.5/=** sawa na **asilimia 29. Shilingi 963,000,000/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, na hadi kufika Machi 2024 **Shilingi 276,043,314.15/=** zilipatikana sawa na **asilimia 29** na **Shilingi 2,122,599,000/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya

mishahara. Hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,677,308,922/=** sawa na **asilimia 79** ya makadirio. Vile vile, program hii ilipangiwa **Shilingi 7,000,000,000/=.** Kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maendeleo na hadi kufikia Machi 2024 imepata **Shilingi 1,614,654,371/=** sawa na **asilimia 23**. Aidha, Programu hii ilitakiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 950,000,000/=** na hadi kufikia Machi 2024 imekusanya jumla ya **Shilingi 772,605,586/=** sawa na **asilimia 81.3** (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D**)

## II. PROGRAMU YA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

40. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuratibu na kusimamia shughuli za utalii nchini. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii endelevu na wenye tija kwa maslahi ya nchi na wananchi. Huduma zinazotolewa katika programu hii ni kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na mipango ya utalii. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Utalii.

## UTEKELEZAJI HALISI

41. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii kwa kushirikiana na wadau wa utalii nchini, imetoa mafunzo ya utembezaji watalii kwa watembeza watalii wasio rasmi (beach boys/girls), kwa ajili ya kuwarasimisha ili waingie kwenye mfumo rasmi wa kuendesha shughuli za kiutalii kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi. Katika mafunzo hayo jumla ya watembeza watalii wasio rasmi 47 wanaendelea na taratibu za kupatiwa vitambulisho vya kutembeza watalii kutoka Kamisheni ya Utalii Zanzibar, pamoja na kutambuliwa na Jumuiya ya

Watembeza watalii Zanzibar (ZATOGA). Kuongezeka kwa watembeza watalii walio rasmi nchini kunaongeza idadi ya ajira kwa wananchi kupitia sekta ya Utalii.

42. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuondoa changamoto katika sekta ya utalii nchini, Idara imeshiriki katika operesheni ya kudhibiti kero ya muziki katika mikoa mitatu ya Unguja na kuweka mazingira mazuri kwenye mahoteli. Shughuli hii imefanywa kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wawekezaji kwenye Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI), Kamisheni ya Utalii na Baraza la Sanaa, Filamu na Utamaduni (BASSFU), ambapo katika operesheni hiyo baadhi ya kumbi za muziki ambazo hazikufuata taratibu zilichukuliwa hatua za kisheria ikiwa pamoja na kufungiwa kwa kumbi hizo na kutoleshwa faini. Aidha, imendelea kutoa elimu na kuwahamasisha wamiliki wa mahoteli kufuata taratibu na sheria zilizowekwa katika kuendesha shughuli za utalii nchini.

43. **Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuimarisha kiwango cha utoaji huduma na ukarimu kwa wageni wanaoingia nchini, Idara ya Utalii imeratibu mafunzo ya Walimu wa Walimu (Trainers of Trainees) kwa kuwasomesha vijana mafunzo ya Uanagenzi 'Apprenticeship' katika utalii na ukarimu kupitia mpango unaondaliwa na Wizara kwa kushirikiana na taasisi ya NTZ Solutions ya Oman. Jumla ya Walimu wa Walimu 22 wamepatiwa mafunzo hayo na kufanikiwa kuhitimu.

44. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imefanya shughuli ya upandaji miti kwenye eneo la kivutio kipya cha utalii cha kisiwa Ndege kilichopo kijiji cha Shumba Mjini Kisiwani

Pemba. Shughuli hii imefanyika kwa kushirikiana na Kamati ya Utalii ya Wilaya ya Micheweni pamoja na wakulima wanaofanya shughuli za kilimo katika kisiwa hicho. Kazi hii imefanyika kwa lengo la kukitunza na kukihifadhi pamoja na kuwahifadhi ndege wanaoishi kwenye kisiwa hicho cha utalii. Kuongezeka kwa vivutio vipya vya utalii Pemba kunapelekea kukamilika kwa dhamira ya kukifungua kisiwa hicho kwenye sekta ya Utalii.

45. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utalii imeweza kuutangaza Utalii wa Zanzibar kwa wajumbe takriban 1,000 waliohudhuria Mikutano mbalimbali ya jumuiya za Kitaifa na Kimataifa waliohudhuria mikutano kwa mwaka 2023/2024 miongoni mwa mikutano hiyo ni Mkutano wa ‘International Development Association’ (IDA 20), Mkutano wa Jumuiya ya Madola 2023, Mkutano wa Jumuiya ya Polisi Wanawake na Chuo cha Taifa cha Ulinzi, kupitia mikutano hiyo wajumbe walipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya vivutio vya Utalii na hivyo kufanya soko la utalii wa ndani na nje kuongezeka.

46. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeandaa shughuli ya usafi katika maeneo ya kitalii Unguja na Pemba, ambayo ilishirikisha wadau mbalimbali wa sekta binafsi na Sekta ya Umma kwa lengo la kuweka mazingira bora ya usafi kwenye maeneo hayo ikiwemo fukwe na kushajiisha usafi nchini kote.

47. **Mheshimiwa Spika,** Idara imeratibu mikutano ya wadau kuzungumzia namna bora ya kuendesha utalii iliyoshirikisha wadau wa sekta binafsi na sekta ya umma, ikiwemo mikutano ya Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo

ya Kale na wawekezaji katika sekta ya utalii, ambayo ilionesha changamoto kadhaa na namna ya kutatuliwa kwa ushirikiano ambapo hatua za utekelezaji kwa baadhi yake zimefanyika na nyengine zinaendelea.

48. **Mheshimiwa Spika**, Idara ya Utalii imeshiriki katika vikao vya kuratibu itifaki za kimataifa zinazohusiana na sekta ya Utalii zilizoandaliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha Zanzibar inashirikishwa katika itifaki hizo ambazo zinasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

49. **Mheshimiwa Mwenyeketi,** Idara ya Utalii imefanya Utafiti mdogo (survey) juu ya changamoto za uhaba wa maji safi na salama na nishati ya umeme kwenye mahatoli kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji ZAWA na Shirika la Umeme Zanzibar ZECO. Utafiti huu wenye lengo la kuzipatia ufumbuzi changamoto za maji na umeme, umefanyika katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na utaendelea kwa maeneo mengine.

50. **Mheshimiwa Spika,** katika kuifanikisha dhana ya Utalii kwa Wote, Idara imeratibu ziara za kutembelea vivutio vya utalii kwa watu wenye mahitaji maalumu kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, kwa ajili ya kuwashirikisha kwenye shughuli za kitalii na kuzitambua fursa za utalii wanazoweza kufaidika nazo. Jumla ya watu wenye mahitaji maalumu 50 wameshiriki katika ziara hiyo. Aidha, Idara imetoa elimu kwa wanajamii wa kijiji cha Vitongoji Kibokoni na kijiji cha Shumba Mjini Micheweni Pemba, kwa lengo la kuwapa elimu ya utalii wanajamii hao wanaoshi karibu na maeneo ya vivutio vya utalii ili waweze kuvitunza vivutio hivyo.

Vile vile, Idara imeandaa na kurusha hewani vipindi vinne kupitia vyombo vya habari vifuatavyo, ZBC TV vipindi viwili, ZCTV kipindi kimoja na TBC kipindi kimoja.

51. **Mheshimiwa Spika,** katika kuweka mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi, Idara imeipatia vitendea kazi vya ofisi ikiwemo kompyuta, vifaa vya kuandikia pamoja na ununuzi wa pikipiki ili kuleta ufanisi wa kazi. Aidha, Idara imelipa stahiki za muda wa ziada kwa wafanyakazi saba.

52. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 411,800,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **Shilingi 121,747,999.26/=** sawa na **asilimia 30.** Jumla ya **Shilingi 246,877,000/=** ziliidhinishwa kwa ajili ya Mishahara na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **Shilingi 188,530,889/=** sawa na **asilimia 76** (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C**).

## III. PROGRAMU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI UTALII

53. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

54. **Mheshimiwa Spika,** huduma inayotolewa katika programu hii ni kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi ili Zanzibar itambulike zaidi kuwa ni kituo bora cha utalii duniani.

## UTEKELEZAJI HALISI

55. **Mheshimiwa Spika,** katika kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi Kamisheni ya utalii imeshiriki maonesho ya utalii ya kimataifa ya ITB (Internationale Tourismus Börse) - Berlin, maonesho ya wazi (Road show) katika nchi za Ujerumani (Cologne), Uholanzi (Amsterdam), Ubelgiji (Brussels) na Italy. Aidha, Kamisheni pia imeshiriki katika ziara za viongozi katika nchi ya Korea ya Kusini. Vile vile, katika kuhamasisha utalii wa ndani Kamisheni ya Utalii imeshiriki katika maonesho ya Swahili Expo (SITE) - Dar Es Salaam, maonesho ya Kili Karibu Fair – Arusha, maonesho ya Kilimo - Nane Nane – Kizimbani, maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Saba Saba) mjini Dar Es Salaam pamoja na Tamasha la Kizimkazi. Aidha, Kamisheni ya Utalii iliandaa Tamasha la Utalii na Utamaduni "Pemba Tourisport Bonanza and Culture" ambalo lilijumuisha michezo na shughuli mbali mbali za utalii ikiwemo mchezo wa ng'ombe, resi za ngalawa, mashindano ya dufu, paredi ya punda, ngoma za asili, ziara katika maeneo ya utalii, kuogelea, triathlon (kuogelea, kupanda baiskeli na kukimbia) na Duathlon (kukimbia na kupanda baiskeli).

56. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii ilipokea ujumbe wa watu wawili kutoka uongozi wa "Aviation Development" uliokuja nchini kufanya ukaguzi juu ya maandalizi ya mkutano wa "Aviation Development" ambao unatarajiwa kufanyika mwaka 2025 hapa Zanzibar. Kufanyika kwa mkutano huu nchini kutasaidia kuitangaza nchi katika utalii wa mikutano, ambapo kutaendgeza idadi ya wageni pamoja na kukuza pato la nchi.

57. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuitangaza nchi kimataifa, Kamisheni ya Utalii imepokea ujumbe wa watu 40 kutoka China wakiwemo waandishi wa habari, wafanya biashara na watu mashuhuri. Ujumbe huo ulikuwa na lengo la kutafuta fursa za biashara pamoja na kuitangaza Zanzibar katika soko la China.

58. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii ilizindua Kampeni ya Kijani na Azimio la Utalii Endelevu (Greener Zanzibar Campaign & The Zanzibar Sustainable Tourism Declaration) mnamo tarehe 9 Februari 2023 katika Maonesho ya Kimataifa ya Zanzibar Tourism Investment & Travel Exhibition. Kampeni hio ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Kampeni hiyo ya Kijani, ni miongoni mwa jitihada za kuendeleza na kuhamasisha wadau wa utalii katika kuchukua hatua za kuendesha biashara kwa njia ya utalii endelevu unaozingatia uhifadhi wa mazingira. Hadi sasa Kamisheni ya Utalii imeweza kuandaa warsha mbili za kuhamasisha wadau wa utalii ili waendeshe biashara kwa njia ya utalii endelevu.

59. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa utalii imeendelea kuchukua hatua ya kuvitangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii waliongia hapa nchini mwaka 2023 ambapo katika mwaka huo idadi ya watalii walioingia nchini iliongezeka kwa asilimia 16 kutoka watalii 548,503 mwaka 2022 hadi kufikia watalii 638,498 mwaka 2023.

60. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi **890,410,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **shilingi 313,756,464/=** sawa na **asilimia 35.** (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C**).

## IV. KURATIBU NA KUSIMAMIA MAENDELEO YA UTALII

61. **Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii na kuweka mazingira bora ya rasilimali katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu hii imeundwa na programu ndogo mbili ambazo ni:

    i. Utawala, Rasilimali Watu na Mipango

    ii. Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii

62. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango inatekelezwa na Idara ya Rasilimali Watu, Mipango na Utawala.

## UTEKELEZAJI HALISI

63. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa za kutosha za watalii wanapoingia nchini Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Maliasili na Utalii, Idara ya Uhamiaji na Ofisi ya Taifa ya Takwimu wanaendelea na utafiti wa utokaji wa wageni (Visitors Exit Survey) kwa mwaka 2023 ambapo ripoti imeshawasilishwa kwa viongozi wa taasisi husika ili kupata ridhaa yao kabla ya kuendelea na zoezi la machapisho. Utafiti huo utapelekea kufahamu baadhi ya

viashiria muhimu vya upimaji wa ukuaji wa sekta ya utalii ikiwemo matumizi ya mtalii kwa siku pamoja na siku zao za ukaazi.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuweka mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi Kamisheni ya Utalii imehakikisha kuwa huduma mbali mbali za uendeshaji wa ofisi zinapatikana pamoja na wafanyakazi kupatiwa stahiki zao. Aidha, safari za kikazi za ndani pamoja na vikao vya mashirikiano na taasisi mbali mbali za Tanzania Bara vimefanyika. Vile vile, Kamisheni ya Utalii imewapatia mafunzo wafanyakazi wake watatu ambapo wafanyakazi wawili wanaendelea na masomo ya shahada ya pili katika fani ya Uongozi wa Utalii katika Chuo cha Harbin University of Commerce nchini China na mmoja anaendelea na masomo ya Shahada ya Pili katika fani ya Masoko na Uhusiano wa Kimataifa katika Chuo cha Uhasibu Tanzania.

**65.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 program ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,885,985,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2024, imefanikiwa kupata **Shilingi 885,744,760.5/=** sawa na **asilimia 46. Shilingi 1,725,888,120/=** kwa ajili ya Mishahara na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **Shilingi 1,221,515,480/=** sawa na **asilimia 70** na kutakiwa kukusanya jumla ya **shilingi 10,295,888,120/=** na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **shilingi 6,136,538,020/=** zimekusanywa sawa na **asilimia 59.6** (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D**).

**66.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii inatekelezwa na Idara ya

Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii yenye jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya utalii nchini.

## UTEKELEZAJI HALISI

67. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imeendelea kufanya ukaguzi wa miradi ya biashara za utalii ili kujiridhisha na huduma zinazotolewa pamoja na kubaini miradi inayofanya biashara kinyume na Sheria ya Utalii. Kazi hiyo imefanyika katika Mikoa yote ya Zanzibar. Katika ukaguzi huo, jumla ya miradi mipya ya utalii 179 imekaguliwa. Miradi hiyo imejumuisha hoteli, mikahawa, michezo ya baharini na kampuni za kuandaa misafara ya watalii. Pamoja na mambo mengine, ukaguzi huo uliangalia mambo mbali mbali kama vile idadi ya vyumba na wafanyakazi, huduma zinazotolewa pamoja na kutoa ushauri wa uendeshaji bora wa biashara hizo.

68. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii imewafanyia mahojiano (interview) watembezaji watalii 80 wapya watakaojishughulisha na kutembeza watalii hapa nchini. Aidha, mafunzo maalumu ya kufanya usafi na kutunza mazingira yalitolewa kwa wajasiri amali 32 wanaokwenda kufanya kazi zao katika mafungu ya mchanga yalioko baharini kama vile fungu Nakupenda lililopo Shangani mjini Unguja.

69. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuifungua zaidi Pemba kiutalii, Kamisheni ya Utalii Zanzibar, imezipandisha hadhi (upgrading) miradi 34 ya viwango mbali mbali ya kulaza wageni kulingana na huduma zinazotolewa katika hoteli hizo. Kupandishwa hadhi kwa miradi hiyo,

kutachochea kuongezeka kwa watalii wenye hadhi ya juu watakaotembelea Pemba.

70. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwaelimisha wananchi juu ya fursa zinazopatikana katika sekta ya utalii na kuwa na utalii endelevu unaochochea uchumi wa buluu, Kamisheni ya Utalii imeandaa na kurusha vipindi mbali mbali kupitia vyombo vya habari vya Redio na Televisheni. Jumla ya vipindi 36 vimerushwa kupitia redio na televisheni ambavyo ni ZBC redio vipindi 13, ZBC TV vipindi vitano, ZCTV vipindi vinne, Bahari FM vipindi viwili na Furaha FM vipindi 12.

71. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ulinzi na usalama wa wageni na mali zao pamoja na sekta ya utalii kwa jumla, Kamisheni ya Utalii kupitia Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia wamefanya doria maalumu 105 katika Mikoa yote mitatu ya Unguja kwa lengo la kuimarisha ulinzi na kuelimisha wananchi juu ya maeneo yanayokubalika kufanyika biashara za utalii. Miongoni mwa maeneo ambayo doria hiyo imefanyika ni pamoja na maeneo ya Mji Mkongwe, Uwanja wa Ndege, Makunduchi, Jambiani, Paje, Bwejuu, Michamvi, Kizimkazi, Pongwe, Uroa, Matemwe, Pwani Mchangani, Nungwi, Kiwengwa na Kendwa. Kufanyika kwa doria hizo kumepunguza vitendo vya uhalifu katika maeneo hayo kwa kiasi kikubwa.

72. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 program ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 993,605,000/=** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **shilingi 240,718,770/=** sawa na **asilimia 24**. (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C**).

## V. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

**73.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu mipango mikuu, sera na tafiti pamoja na usimamizi na uendeshaji mzuri wa rasilimali watu katika Wizara. Programu hii imeundwa na programu ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale

ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

**74.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** huduma zinazotolewa katika programu ndogo ni kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi, utayarishaji wa ripoti za fedha na ukaguzi pamoja na mpango wa manunuzi.

## UTEKELEZAJI HALISI

**76.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeweza kuwajengea uwezo wafanyakazi wake sita kwa kuratibu mafunzo ya muda mrefu katika fani na ngazi tofauti. (**Tafadhali Angalia Kiambatanisho nambari 2**). Kadhalika, wafanyakazi saba wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya Zanzibar. Aidha,

wafanyakazi 327 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya ndani ya Wizara ikiwemo Kuimarisha Utendaji kazi wa Divisheni ya Kumbukumbu na matumizi ya Ofisi Mtandao (E-Office), Matumizi ya Mfumo wa Manunuzi ya Mtandao, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, Sheria na Kanuni za Fedha pamoja na Sheria na Kanuni za Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali.

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imefanikiwa kuajiri wafanyakazi 6 kwa nafasi mpya pamoja na kujaza zilizokuwa wazi kwa Unguja na Pemba. Ajira hizo zimeiwezesha Wizara kuimarika kwa utendaji kazi katika Idara zake.

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imesimamia ufanyaji wa tathmini ya utendaji kazi wa wafanyakazi wake 268 Unguja na Pemba na kujiridhisha na utendaji wao. Vilevile, Viongozi na Watendaji wa Wizara waliweza kufanya ufuatiliaji wa kazi pamoja na ziara za kikazi Pemba. Aidha, Wizara imeweza kushiriki katika vikao kazi na mikutano ya kiutendaji Tanzania Bara. Pia, Idara imeratibu vikao vya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya Wizara kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa Malengo, Sera, kanuni, Sheria, Miongozo na Miradi mbali mbali ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mashirikiano baina ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Wizara imefanya jumla ya vikao kazi 13 na Wadau wa Utalii na Mambo ya Kale wa ndani na nje ya nchi na kujadili maendeleo ya sekta. Vilevile, katika kuimarisha utekelezaji wa shughuli zake pamoja na kusimamia utekelezaji wa mikataba na maazimio ya Kikanda na Kimataifa, Wizara

imeshiriki katika Kongamano la Kimataifa la 24 kwa Nchi za Visiwa liliofanyika Hainan nchini China, Mkutano wa Kimataifa wa UNESCO ulikofanyika nchini Saudi Arabia. Aidha, Wizara imefanikiwa kufanya Mkutano na Wadau wa Utalii na kuzindua safari za ndege za moja kwa moja kati ya Zanzibar na nchi ya Ureno. Kadhalika, Wizara, imepokea wageni 17 kutoka mataifa mbali mbali na Mashirika ya Kimataifa kwa lengo la kuimarisha uhusiano mwema na mashirikiano ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Nchi hizo ni pamoja na Oman, Afrika ya Kusini, Jamaika, Marekani na China.

**80.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 833,200,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi** 1,053,538,000/= kwa ajili ya Mishahara hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **shilingi 341,630,504.5/=** kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 41** na kupata **shilingi 720,109,833/=** kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 68** (**Tafadhali angalia kiambatisho nambari 1D**).

**81.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya kuratibu na kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la kupanga, kutayarisha, kufuatilia na kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa sera na tafiti, kuandaa na kuwasilisha bajeti ya Wizara, kuandaa na kusimamia mipango na miradi ya maendeleo ya Wizara.

## UTEKELEZAJI HALISI

83. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mashirikiano ya taasisi ya Tony Blair Institute (TBI) ipo katika mchakato wa uandaaji na ukamilishaji wa Rasimu za awali ya Sera ya Utalii, Mpango Mkuu wa Utalii hasa katika kukifungua kisiwa cha Pemba. Rasimu hizi za awali zinategemewa kuwasilishwa kwa wadau wa Utalii wa Unguja na Pemba kwa lengo la kupatiwa maoni na ushauri, ili ziwe bora zaidi. Kukamilika kwa Sera hii pamoja na rasimu zake kutasaidia kuwepo kwa mikakati imara ya uendeshaji na usimamizi wa utalii nchini pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi ya teknolojia duniani.

84. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuimarisha mashirikiano kwa sekta za Utalii, Mambo ya Kale pamoja na Maliasili kati ya SMZ na SMT, Idara imeratibu vikao vya mashirikiano kati ya Wizara husika vilivyofanyika Chake Chake Pemba, ambapo watendaji walijadili fursa na changamoto mbali mbali zinazojitokeza katika utendaji kazi wa kila siku. Majadiliano hayo yaliibuwa maazimio ambayo yameridhiwa na Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara zote tatu waliokutana kwa lengo la kuimarisha mashirikiano kwenye utendaji wa kazi.

85. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi unafanikiwa kama ilivyopangwa, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ambayo ni mradi wa Kuimarisha Eneo la Kihistoria la Mangapwani Unguja na Mradi wa Kuimarisha Eneo la Kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba.

Utekelezaji wa mradi wa eneo la kihistoria la Mangapwani umefikia asilimia 85 na utekelezaji wa mradi wa eneo la kihistoria Ras Mkumbuu umefikia asilimia 40. Uimarishaji wa maeneo ya kihistoria una lengo la kuhifadhi, kutunza na kuendeleza historia kwa faida ya vizazi pamoja na kuongeza vivutio vya utalii.

86. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera, na Utafiti imetayarisha na kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Malengo na Shabaha za Mpango wa Maendeleo wa ZADEP katika sekta za Utalii na Mambo ya Kale kwa Tume ya Mipango, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Aidha, Idara iliratibu uwasilishaji wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (2020-2025) uliowasilishwa katika Ofisi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Kiswandui. Pia, Idara imefanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Malengo na Shughuli zinazotekelezwa na Idara na Taasisi za Wizara. Katika ufuatiliaji huo Idara imejiridhisha kwamba taasisi hizo zinatekeleza shughuli zao kwa mujibu wa Mpango Kazi.

87. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua za kuimarisha utendaji kazi kwa wafanyakazi wake, Idara imegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa mfanyakazi mmoja anaesomea Shahada ya Pili ya Upangaji wa Miradi na Uongozi katika Chuo cha IAA kilichopo Arusha. Aidha, imelipa stahiki ya likizo kwa mfanyakazi mmoja. Vile vile, Idara imewezesha upatikanaji wa vifaa vya Ofisi vikiwemo vifaa vya kuandikia, ununuzi wa mafuta pamoja na kompyuta. Vile vile Idara imefanikiwa kugharamia safari za kikazi kati ya Unguja, Pemba na Dar es Salaam kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi.

**88.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 250,000,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 206,249,000/=** kwa ajili ya Mishahara na hadi kufikia Machi 2024 imefanikiwa kupata **Shilingi 83,014,547.04/=** kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 33** na **Shilingi 162,757,823/=** kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 79** (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C**).

**89.** **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba.

**90.** **Mheshimiwa Spika,** huduma ambazo zinatolewa ni uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba, kuratibu Miradi ya Maendeleo na kujenga uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi.

## UTEKELEZAJI HALISI

**91.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imeendeleza na kushajihisha utalii wa ndani kwa kushirikiana na wadau katika maswala ya utalii wa michezo na kuibua vivutio vipya vya kimaumbile na vya kihistoria vilivyopo kisiwani Pemba katika kijiji cha Maziwa Ngo'mbe Wilaya ya Micheweni Pemba. Aidha, Ofisi Kuu Pemba imeendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje katika suala zima la kuutangaza utalii kupitia vyombo vya habari kwa kufanya makala za kutangaza vivutio vya utalii na fursa zilizopo kupitia sekta ya utalii.

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imefanya ziara maalumu kwa viongozi wa Serikali na waandishi wa

habari katika kuvielewa na kuvitangaza vivutio vya utalii vikiwemo maeneo ya kihistoria ya Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba. Aidha, Ofisi Kuu Pemba imefanya ufuatiliaji wa shughuli za Wizara, ufuatiliaji wa miradi inayoendelea kutekelezwa na miradi mipya inayotarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025.

93. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imegharamia mafunzo ya wafanyakazi watatu, katika ngazi ya Shahada ya Uzamili wafanyakazi wawili katika fani ya Uchumi na Utawala na mfanyakazi mmoja kwa ngazi ya Stashahada katika fani ya Utunzaji Kumbukumbu. Aidha, Ofisi Kuu imegharamia mafunzo ya awali (Induction Course) kwa mfanyakazi mmoja mpya, pamoja na kuwapatia mafunzo ya vitendo wanafunzi sita kutoka Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya katika ngazi ya Cheti na Stashahada katika fani ya Mapokezi na Ukarimu.

94. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imeimarisha Mazingira ya Ofisi kwa kupatikana nyenzo za kufanyia kazi kama vitendea kazi, zikiwemo kompyuta mbili, Huduma za mawasiliano, mafuta pamoja na Vifaa vya kuandikia. Aidha, wafanyakazi 20 wamepatiwa stahiki zao ikiwemo huduma ya likizo kwa wanyakazi 14, wafanyakazi 6 wamelipwa posho la baada ya saa za kazi, na kulipia safari kikazi kwa watendaji mbali mbali wanaosafiri kwenda Unguja na Tanzania Bara.

95. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 897,637,000/=** Mishahara ni **shilingi 497,637,000/=** na **shilingi 400,000,000/=** ni kwa ajili ya kazi za kawaida na

hadi kufikia Machi 2024, Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kupata **shilingi 515,849,594/=**, ikiwa misharaha ni **Shilingi 381,597,829/=** sawa na **asilimia 77** na kazi za kawaida ni **shilingi 134,251,765/=** sawa na **asilimia 34.** Programu ndogo hii imetakiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 50,000,000/=,** na hadi kufikia Machi 2024, jumla ya **Shilingi 2,463,000/=** zimekusanywa sawa na **asilimia 5** (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1C na 1D**).

## G. VIPAUMBELE VYA WIZARA KWA MWAKA 2024/2025.

**96.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale pamoja na mambo mengi imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuizindua Sera ya Taifa ya Makumbusho na Urithi wa Mambo ya Kale ya Mwaka 2023.

ii. Kuifanyia mapitio Sheria ya Utalii ya mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2012.

iii. Kuongeza wigo wa bidhaa za utalii

iv. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria

v. Kuandaa Mpango Mkuu wa Utalii wa Kisiwa Cha Pemba ‘Pemba Tourism Master Plan’.

vi. Kufanya matengenezo ya baadhi ya nyumba zilizopo katika hali mbaya ndani ya eneo la Mji Mkongwe

vii. Kuendelea kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza katika maeneo ya kihistoria.

viii. Kuendelea kuiimarisha kikosi cha Polisi Utalii ili kuweza kutoa huduma bora.

## H. MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**97. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Wizara ya Utalii, na Mambo ya Kale imepangiwa jumla ya **Shilingi 47,032,992,000/=** Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,418,800,000/=** ni kwa matumizi ya kawaida, **Shilingi 4,588,370,000/=** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 39,025,822,000/=** kwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara imepangiwa kukusanya mapato yanayokwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali **Shilingi 1,239,894,000/=.** (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1E, 1F, 1G**).

**98. Mheshimiwa Spika,** katika fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni **Shilingi 8,007,170,000/=, Shilingi 3,500,200,000/=** ni mishahara kwa taasisi za Wizara zisizo za ruzuku, **Shilingi 3,043,200,000/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa taasisi za Wizara zisizo za ruzuku. Aidha, **Shilingi 1,088,170,000/=** ni kwa ajili ya mishahara kwa Taasisi za Wizara zinazopokea ruzuku na **Shilingi 375,600,000/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa taasisi za Wizara zinazopokea ruzuku. (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F**).

**99. Mheshimiwa Spika,** katika fedha za miradi ya maendeleo **Shilingi 39,025,822,000/=** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria pamoja na ukarabati wa baadhi ya nyumba hatarishi zilizopo ndani ya eneo la Hifadhi ya Mji Mkongwe. (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F**).

100. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Utalii inatarajia kukusanya **Shilingi 12,825,262,611/=**, kati ya hizo **Shilingi 5,000,000,000/=** zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, **Shilingi 2,455,878,177/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 5,369,383,900/=** kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida.

## I. KUWASILISHA BAJETI YA MFUMO WA PROGRAMU (PROGRAM BASED BUDGET - PBB) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

101. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 47,032,992,000/=** kwa ajili ya kutekeleza programu kuu tatu ambazo ni: -

i. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe. (**Shilingi 42,625,419,000/=**)

ii. Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii. (**Shilingi 1,152,962,000/=)**

iii. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii. (**Shilingi 972,130,000/=**).

iv. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii. (**Shilingi 11,853,133,000/=**).

v. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. (**Shilingi 3,254,612,000/=**). (**Tafadhali angalia kiambatisho namba 1F**)

**Programu ya kwanza: Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe**

102. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inatekelezwa na Idara ya Makumbusho pamoja na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Programu hii ina jukumu la kuhakikisha kwamba maeneo ya Kihistoria na Mambo ya Kale yanaendelezwa kwa kuhifadhiwa, kulindwa na kutangazwa pamoja na kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe ili uendelee kubaki kuwa urithi wa dunia kwa kutoa faida kwa kizazi cha sasa na baadae. Aidha, matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni Kuyaimarisha Maeneo ya Kihistoria pamoja na kuuendeleza Mji Mkongwe. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 42,625,419,000/=.**

103. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuyahifadhi na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria kwa kuyawekea uzio na kuyaimarisha kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

ii. Kuendelea na kuimarisha jitihada za kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika maeneo ya kihistoria.

iii. Kuzifanya rasilimali za historia na urithi wa utamaduni kuwa kichocheo cha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia shughuli za Utalii.

iv. Uelimishwaji kwa kuishirikisha jamii katika uhifadhi wa maeneo ya kihistoria na Urithi wa Utamaduni.

v. Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu na kusimamia Uhifadhi wa Majengo na maeneo ya Mji Mkongwe.

vi. Kuimarisha maeneo, majengo na miundombinu ndani ya Mji Mkongwe.

vii. Kuutangaza Mji Mkongwe kitaifa na kimataifa.

viii. Kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

104. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **shilingi 1,025,600,000/=** kwa kazi za kawaida, **shilingi 2,573,997,000/=** kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi 39,025,822,000/=** kwa kazi za Maendeleo. Pia, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe Makusanyo ya Programu hii ya **Shilingi 1,189,894,000/=**.

**Programu ya Pili: Programu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii**

105. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii inatekelezwa na Idara ya Utalii. Jukumu la msingi katika programu hii ni Kusimamia na Kuratibu shughuli za Utalii pamoja na Kuwahamasisha Wananchi juu ya Dhana ya Utalii kwa Wote. Matokeo ya muda mrefu ni kuwa na utalii wenye kuleta manufaa kwa wananchi. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Uratibu na Uendelezaji wa shughuli za Utalii. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 1,152,962,000/=.**

106. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuibua na kuviendeleza vivutio vipya vya utalii nchini.

ii. Kuzishirikisha Kamati za Utalii za Wilaya pamoja na wananchi katika kuendeleza dhana ya Utalii kwa Wote.

iii. Kusimamia ushiriki wa Zanzibar katika itifaki za kitaifa na kimataifa zinazohusiana na sekta ya utalii ikiwemo zinazoratibiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taasisi nyengine za kitaifa na kimataifa.

iv. Kuratibu mikutano ya wadau yenye lengo la kuzungumzia namna bora ya kuendesha utalii itayoshirikisha wadau wa sekta binafsi na sekta ya umma ili kuondoa kwa ushirikiano changamoto zilizopo na kushirikisha wadau katika maendeleo ya sekta ya utalii nchini.

v. Kuratibu na kushajiisha harakati za maendeleo endelevu ya utalii yenye kuzingatia uhifadhi wa mazingira na usafi katika maeneo ya kitalii Unguja na Pemba.

vi. Kuimarisha utolewaji huduma bora za utalii wa kiwango cha juu kwa kuelimisha wadau ikiwemo wenye kuandaa misafara ya utalii, watembeza watalii, wajasiriamali wa bidhaa za utalii na waendesha mashamba ya viungo.

vii. Kukiimarisha kitengo cha polisi Utalii na Diplomasia ili kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi

107. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, ninawaomba Wajumbe

wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 879,000,353/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 273,961,647.29/=** kwa ajili ya Mishahara.

**Programu ya Tatu: Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii**

**108. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu hii ni kuongeza uelewa kwa wakazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusu bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar. Programu inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

**109. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo : -

i. Kuandaa na kushiriki katika maonyesho, mikutano na makongamano ya utalii ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuvutia wageni kuvitembelea vivutio vya utalii vya Zanzibar.

ii. Kuwekeza katika utalii wa mikutano (MICE) pamoja na utalii wa urithi wa kihistoria

iii. Kuwaalika waandishi wa habari za utalii wa kimataifa, wamiliki wa mitandao ya kijamii na watu mashuhuri ili Zanzibar ipate fursa ya kutangazwa kupitia watu hawa kwa gharama nafuu.

**110. Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2024/2025, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha makusanyo

yatakayotumiwa na programu hii ambayo ni jumla ya **Shilingi 972,130,000 /=** kwa kazi za kawaida.

**Programu ya Nne: Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii**

**111. Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuongeza tija ya Sekta ya Utalii na kuweka mazingira bora na rasilimali watu katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera na mipango ya utalii. Programu hii itatekelezwa na Kamisheni ya Utalii, ambayo itakuwa na programu ndogo mbili nazo ni: -

i. Utawala, Rasilimali Watu na Mipango

ii. Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii

**112. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango, inatekelezwa na Idara ya Rasilimali Watu, Mipango na Utawala. Programu ndogo hii ina lengo la kupanga na kuimarisha uwezo wa Kamisheni ili iweze kutekeleza majukumu yake.

**113. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu ndogo ya Utawala, Rasilimali Watu na Mipango inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuitangaza Zanzibar kitaifa, kikanda na kimataifa

ii. Kufanya tafiti wa utokaji wa wageni ili kufahamu baadhi ya viashiria muhimu vya upimaji wa ukuaji wa sekta ya utalii ikiwemo matumizi ya mtalii kwa siku.

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu

iv. Kuandaa na kuendesha vikao vya Makamishna na Wadau wa Utalii

v. Kufanya tathmini na kufuatilia shughuli za Kamisheni ya Utalii na Miradi ya Maendeleo.

vi. Kufanya Tathmini ya Rasilimali Watu katika Kamisheni ya Utalii

**114. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2024/2025, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo yatakayotumiwa na programu ndogo hii, ambayo ni **Shilingi 3,152,071,900/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 2,455,878,711/=** kwa ajili ya mishahara. Pia, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo ya Programu hii ya **Shilingi 5,000,000,000/=** zitakazoingia Mfuko Mkuu wa Hazina.

**115. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu na Shughuli za Utalii, inatekelezwa na Idara ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii. Programu ndogo hii ina lengo la kusimamia na kuratibu maendeleo ya Utalii nchini kwa kushajihisha uwekezaji vitega uchumi katika sekta ya Utalii Zanzibar.

**116. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukagua na kufuatilia miradi ya utalii ili kuhakiki huduma zinazotolewa.

ii. Kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu sekta ya Utalii pamoja na fursa zinazopatikana kwa kutumia radio, televisheni na makongamano.

iii. Kuandaa mafunzo kwa maofisa watakaofanya kazi ya kuweka viwango vya madaraja kwa bidhaa za utalii kwa vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

117. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo yatakayotumiwa na Programu ndogo hii ya **Shilingi 743,910,000/=** kwa kazi za kawaida.

**Programu ya Tano: Uendeshaji na Mipango katika Sekta yaUtalii na Mambo ya Kale**

118. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu katika Wizara. Matokeo ya muda mrefu ya programu hii ni kuwepo kwa Usimamizi Bora wa Mipango na Uendeshaji wa Rasilimali Watu katika Wizara. Programu hii imepangiwa jumla ya **Shilingi 3,254,612,000/=** na itasimamia programu ndogo tatu ambazo ni: -

i. Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale. (**Shilingi 1,776,656,000/=**)

ii. Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara. (**Shilingi 484,242,000/=**)

iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba. (**Shilingi 993,714,000/=**)

**119. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ambayo ina jukumu la Kusimamia shughuli zote za Utawala, Utumishi, Maendeleo, Wajibu na Maslahi ya Wafanyakazi wa Wizara.

**120. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali Watu wa Wizara. Huduma zinazotarajiwa kutolewa ni Kujenga uwezo na Mazingira Mazuri ya Kazi kwa Wafanyakazi na Usimamizi wa Mpango wa Manunuzi na Fedha.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kuimarisha ufanisi na utendaji kazi pamoja na kuweka mazingira mazuri wa kufanya kazi kwa kuzingatia afya na usalama kazini.

ii. Kupima utendaji kazi wa wafanyakazi wa Wizara.

iii. Kusimamia Utekelezaji wa Mpango na Manunuzi kwa kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na Sheria na Kanuni ya Fedha.

iv. Kuimarisha mashirikiano na mahusiano mema baina ya Wizara na Wadau ikiwemo Taasisi, Mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa ajili ya Maendeleo ya Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

122. **Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2024/2025, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 833,200,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 943,456,000/=** kwa ajili ya Mishahara.

123. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti yenye jukumu la Kupanga, Kutayarisha, Kuratibu, Kufuatilia na Kutathmini Mipango, Sera, Tafiti na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

124. **Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti za Wizara. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera na Tafiti, Kuratibu, Kuandaa Bajeti pamoja na Kuratibu na Kusimamia Mipango na Miradi ya Maendeleo ya Wizara.

125. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Utalii ya mwaka 2017

ii. Kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Wizara kwa kufuatilia na kutathmini kazi zinazofanyika.

iii. Kuratibu Vikao vya Ushirikiano kwa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale kati ya SMZ na SMT.

iv. Kuandaa maandiko ya miradi yatakayosaidia kupata ufadhili wa miradi inayotekelezwa na Wizara.

**126. Mheshimiwa Spika,** ili programu ndogo iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla **Shilingi 250,000,000/=** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 234,242,000/=** kwa ajili ya Mishahara.

**127. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba, ina jukumu la Kuhakikisha kuwa Majukumu, Malengo na Shughuli zote za Wizara zilizopangwa zinatekelezwa kwa ufanisi kwa upande wa Pemba.

**128. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la programu ndogo hii ni Kusimamia na Kuratibu shughuli za Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Wizara katika Ofisi Kuu-Pemba. Huduma ambazo zinatarajiwa kutolewa ni Uratibu wa Sera, Tafiti na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu-Pemba, Kuratibu Miradi ya Maendeleo na Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi na Mazingira mazuri ya kazi.

**129. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025 programu ndogo hii inategemea kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuratibu shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba.

ii. Kuibua vivutio vipya vya utalii na kuviendeleza vilivyopo kwa upande wa Pemba

iii. Kuhamasisha utalii wa ndani wenye tija kwa wananchi

iv. Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Malengo na Miradi inayotekelezwa Pemba.

v. Kuratibu Matamasha ya Utalii yatakayofanyika Pemba.

vi. Kuwapatia wafanyakazi vitendea kazi vya kutosha ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

130. **Mheshimiwa Spika,** ili programu hii iweze kutekelezwa kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2024/2025, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 431,400,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 562,314,000/=** kwa ajili ya Mishahara. Aidha, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo kwa programu ndogo ya **Shilingi 50,000,000/=** zitakazoingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

## J. SHUKURANI

131. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kumaliza hotuba yangu, naomba kutoa shukurani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuniamini kuwa Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na kuitumikia nafasi ya Uwaziri katika Wizara hii ya Utalii na Mambo ya Kale, naahidi kwamba nitatumia jitihada zangu zote, maarifa na

uwezo nilopewa na Mwenyezi Mungu katika kuitumikia nafasi hii kwa maslahi mapana ya nchi. Aidha, nimshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyeketi wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kutupa Ushauri, Miongozo na Maelekezo katika kuziendeleza sekta hizi za Utalii na Mambo ya Kale kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi na kuinua kipato kwa wananchi. Nitumie fursa hii kumuomba Mwenye enzi Mungu amjaalie Rais wetu, Afya njema, Hekima, Busara na Uwezo wa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar katika kuwaletea maendeleo.

132. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kutoa shukurani za kipekee kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi imara kabisa wa Taifa letu na hasa katika mwaka huu adhimu ambapo tumeadhimisha Miaka 60 ya Mapinduzi na Muungano wetu. Mheshimiwa Rais Samia amekuwa mstari wa mbele na kinara mkuu wa Jamhuri yetu katika kuutangaza na kwa mafanikio makubwa kabisa Utalii na Urithi Wetu wa Tanzania na ikiwemo Zanzibar kupitia programu mbali mbali kama zile za Royal Tour na Presidential Tour.

133. **Mheshimiwa Spika,** shukurani maalumu ziwaendee watendaji Wakuu wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini Pemba, Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe, Wakurugenzi pamoja na Wakuu wote wa Taasisi za Wizara kwa kunipa ushirikiano wa kutosha katika kipindi hiki kifupi ambacho nimekuwepo Wizarani, naamini kwamba mashirikiano haya

ninayoyapata yataniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi zaidi. Vile vile, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wote wa Wizara hii Unguja na Pemba kwa kuendelea kufanya kazi katika hali ya ubora na umakini wa hali juu, jambo ambalo linapelekea kufanikiwa kwa utekelezaji wa shughuli na malengo ya Wizara. Hali hii inanipa faraja na imani ya utekelezaji kwamba kuweza kuvuka Malengo na Maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ifikapo 2025.

134. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale wa Unguja na Pemba kwa jinsi tunavyoendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha sekta hizi zinapata maendeleo makubwa na kwa haraka. Aidha, nitumie hadhira hii, kuwashukuru wamiliki wa vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa pamoja na mitandao ya kijamii, kwa kazi kubwa yenye ubora wa hali ya juu wanayoifanya ya kusaidia kuitangaza Zanzibar pamoja na vivutio vya utalii vilivyomo nchini. Kufanya hivyo kumesaidia kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini na kukuza pato la nchi.

135. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kuzishukuru taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa katika utekelezaji wa vipaumbele vyetu vya Utalii na Mambo ya Kale. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais (Ikulu); Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ikiwemo Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao wamekuwa karibu sana nasi

katika kulipeleka mbele gurudumu letu la utalii endelevu; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji ikiwemo ZIPA; Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Wizara ya Afya; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

136. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee ninapenda kuishukuru Wizara ya Fedha pamoja na Tume ya Mipango kwa kutuwezesha kupata fedha kwa ajili ya kufanikisha Malengo na shughuli za Wizara. Aidha, niwashukuru tena kwa kuiridhia Kamisheni ya Utalii pamoja na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kuweza kutumia fedha wanazozikusanya katika vyanzo vyao vya mapato pamoja na kurudisha gawio katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Kufanya hivyo kumeiwezesha Kamisheni ya Utalii na Mamlaka ya Mji Mkongwe kuongeza juhudi za kuitangaza nchi kitaifa, kikanda na kimataifa pamoja na kuimarisha utendaji kazi.

137. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Ulinzi na Usalama, Baraza la Biashara la Taifa, Majukwaa ya Vijana, Polisi Utalii na Vikosi vya SMZ na vyombo vya Habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu.

138. **Mheshimiwa Spika,** naomba uniruhusu nizishukuru Nchi, Mashirika na Taasisi ambazo zimeshirikiana kwa karibu na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, pamoja na wadau mbali mbali katika kufanikisha kutekeleza Malengo na Majukumu ya Wizara kupitia sekta zake mbili. Miongoni mwa nchi hizo ni Afrika ya Kusini, Kenya, Oman, Falme za Kiarabu, Qatar, Morocco, Saudi Arabia, China, Japan, Jamhuri ya Korea, India, Uingereza, Marekani, Canada, Italia, Norway, Sweden, Finland, Denmark, Poland, Ureno, Ujerumani na Ufaransa. Niwashukuru sana Mabalozi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo katika mataifa mbali mbali na wanaoendelea kuitangaza Zanzibar kupitia Diplomasia ya Uchumi.

139. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia inatoa shukrani zake za dhati na za kipekee kwa wadau wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa mipango yake ya Utalii, Mambo ya Kale na Hifadhi ya Mji Mkongwe. Taasisi hizi ni pamoja na Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano; Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki (SMT). Shukurani pekee ziwaendee Waheshimiwa Mabalozi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walio mstari wa mbele katika kuutangaza Utalii na Urithi wetu kote duniani.

140. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, tunapenda kuyashukuru Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNDP, UNESCO, UNICEF, UNECA, na UNWTO. Tunalishukuru Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID)

kupitia miradi yake ya Heshimu Bahari na Uwezeshaji wa Jamii. Benki ya Dunia, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi (IORA). Kwa umuhimu wa pekee tunapenda kuzishukuru na kutambua michango ya Jumuiya na Taasisi mbali mbali za maendeleo, kifedha, kiutalii na Mambo ya Kale kama vile TBI, PDB, NMB, PBZ, ZATI, ZATO, ZATOGA, HAZ, TATO, PATI, World Vegetable Center na JUHIMKO.

141. **Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa Utulivu, Umakini na Usikivu wa hali ya juu.

## K. MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA KUTEKELEZA PROGRAMU ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

142. **Mheshimiwa Spika,** ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako kujadili kwa kina matumizi ya jumla ya Wizara ya **shilingi 47,032,992,000/=**. Kati ya hizo **Shilingi 3,418,800,000/=** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 4,588,370,000/=** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 39,025,822,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, naomba Wajumbe wa Baraza lako waidhinishe makusanyo ya mapato ya **Shilingi 1,239,894,000/=** kwa fedha zinazoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

143. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamisheni ya Utalii imeruhusiwa kutumia fedha zinazotokana na makusanyo yake. Hivyo, ninawaomba Wajumbe wa Baraza lako

kuidhinisha makusanyo ya **Shilingi 12,825,262,611/=** ambazo zitakusanywa na Kamisheni ya Utalii, kati ya hizo **Shilingi 5,000,000,000/=** zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, **Shilingi 2,455,878,711/=** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 5,369,383,900/=** kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kawaida.

## L. HITIMISHO

**144. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Waipokee, Waijadili, Watushauri, Watuelekeze na baadae Wapitishe bajeti hii ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

**145. Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.

**Ahsante,**

**Mudrik Ramadhan Soraga (MBM),**

**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale,**
**Zanzibar.**

**Kiambatisho Namba1A**

## TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU

| TASISI | MAELEZO | BAJETI YA JULAI 2023 - 2024 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI - MACHI 2023/2024 |
|---|---|---|---|
| Ofisi kuu Pemba | Mishahara | 497,637,000.00 | 381,597,829.00 |
| | M/Mengineyo | 400,000,000.00 | 134,251,765.00 |
| JUMLA | | 897,637,000.00 | 515,849,594.00 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 206,249,000.00 | 162,757,823.00 |
| | M/Mengineyo | 250,000,000.00 | 83,014,547.04 |
| JUMLA | | 456,249,000.00 | 245,772,370.04 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 1,053,538,000.00 | 720,109,833.00 |
| | M/Mengineyo | 833,200,000.00 | 341,630,504.50 |
| JUMLA | | 1,886,738,000.00 | 1,061,740,337.50 |
| Idara ya Utalii | Mishahara | 246,877,000.00 | 188,530,889.00 |
| | M/Mengineyo | 411,800,000.00 | 121,747,999.26 |
| JUMLA | | 658,677,000.00 | 310,278,888.26 |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Mishahara | 1,285,399,000.00 | 1,030,313,960.00 |
| | M/Mengineyo | 650,000,000.00 | 163,908,314.15 |
| JUMLA | | 1,935,399,000.00 | 1,194,222,274.15 |
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,289,700,000.00** | **2,483,310,334.00** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEO** | | **2,545,000,000.00** | **844,553,129.95** |
| **JUMLA KU KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **5,834,700,000.00** | **3,327,863,463.95** |

## TAASISI ZA RUZUKU

| MAELEZO | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2023 - 2024 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI -MACHI 2023/2024 |
|---|---|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | Mishahara | 837,200,000.00 | 646,994,962.00 |
| | M/Mengineyo | 313,000,000.00 | 112,135,000.00 |
| | | 1,150,200,000.00 | 759,129,962.00 |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **837,200,000.00** | **646,994,962.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **313,000,000.00** | **112,135,000.00** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **1,150,200,000.00** | **759,129,962.00** |
| | | | |
| | | | |
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **4,126,900,000.00** | **3,130,305,296.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **2,858,000,000.00** | **956,688,129.95** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)** | | **6,984,900,000.00** | **4,086,993,425.95** |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | | | |
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria | | **7,000,000,000.00** | **973,626,507.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO)** | | **7,000,000,000.00** | **973,626,507.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **13,984,900,000.00** | **5,060,619,932.95** |

## KAMISHENI YA UTALII

| MAELEZO | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2023 - 2024 | FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI - MACHI 2023/2024 |
|---|---|---|---|
| KAMISHENI YA UTALII | Mishahara | 1,725,888,120.00 | 1,221,515,480.00 |
| | M/Mengineyo | 3,770,000,000.00 | 1,440,219,994.50 |
| | | 5,495,888,120.00 | 2,661,735,474.50 |
| **JUMLA YA MISHAHARA** | | **1,725,888,120.00** | **1,221,515,480.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **3,770,000,000.00** | **1,440,219,994.50** |
| **JUMLA KUU YA KAMISHENI YA UTALII** | | **5,495,888,120.00** | **2,661,735,474.50** |

## Kiambatisho Namba1B

## MAPATO YALIOKUSANYWA JULAI 2023 HADI JUNI 2024
## MAPATO YANAYOINGIA HAZINA

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | MAPATO YALIOKUSANYWA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 700,000,000.00 | 520,168,569.00 | 74.31 |
| Ofisi Kuu Pemba | 50,000,000.00 | 2,203,000.00 | 4.41 |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 250,000,000.00 | 93,320,000.00 | 37.33 |
| **JUMLA NDOGO** | **1,000,000,000.00** | **615,691,569.00** | **61.57** |
| Kamisheni ya Utalii | 9,257,949,000.00 | 6,136,538,020.00 | 66.28 |
| **JUMLA NDOGO** | **9,257,949,000.00** | **6,136,538,020.00** | **66.28** |
| **JUMLA** | **10,257,949,000.00** | **6,752,229,589.00** | **65.82** |

## Kiambatisho Namba1C

## FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI JUNI 2024 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

### Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 8,935,399,000.00 | 2,167,848,781.15 | **24.26** |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 1,150,200,000.00 | 759,129,962.00 | **66.00** |
| **JUMLA** | **10,085,599,000.00** | **2,926,978,743.15** | **29.02** |

### Programu ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Utalii | 658,677,000.00 | 310,278,888.26 | **47.11** |
| **JUMLA** | **658,677,000.00** | **310,278,888.26** | **47.11** |

### Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Masoko) | 890,410,000.00 | 313,756,464.00 | **35.24** |
| **JUMLA** | 890,410,000.00 | 313,756,464.00 | **35.24** |

### Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii(Idara ya Mipango) | 4,605,478,120.00 | 2,347,979,010.50 | **50.98** |
| **JUMLA** | **4,605,478,120.00** | **2,347,979,010.50** | **50.98** |

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 1,886,738,000.00 | 1,061,740,337.50 | **56.27** |
| JUMLA | 1,886,738,000.00 | 1,061,740,337.50 | **56.27** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamisha Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2023/20214 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 456,249,000.00 | 245,772,370.04 | **53.87** |
| JUMLA | 456,249,000.00 | 245,772,370.04 | **53.87** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 897,637,000.00 | 515,849,594.00 | **57.47** |
| JUMLA | 897,637,000.00 | 515,849,594.00 | **57.47** |

**Kiambatisho Namba1D**

## FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2023 HADI JUNE 2024 KWA KILA PROGRAMU NDOGO

**Programu ndogo ya Uendelezaji wa Urithi wa Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 700,000,000.00 | 659,840,586.00 | **94.00** |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 250,000,000.00 | 112,765,000.00 | **45.00** |
| JUMLA | **950,000,000.00** | **772,605,586.00** | **81.32** |

## Programu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii(Idara ya Mipango) | 9,257,949,000.00 | 6,136,538,020.00 | **66.28** |
| **JUMLA** | **9,257,949,000.00** | **6,136,538,020.00** | **66.28** |

## Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba

| TAASISI | BAJETI 2023/2024 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 50,000,000.00 | 2,463,000.00 | **5.00** |
| **JUMLA** | **50,000,000.00** | **2,463,000.00** | **5.00** |

**Kiambatisho Namba1E**

## BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

| MAELEZO | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2024- 2025 |
|---|---|---|
| Ofisi kuu Pemba | Mishahara | 562,314,000.00 |
| | M/Mengineyo | 431,400,000.00 |
| JUMLA | | 993,714,000.00 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | 234,242,000.00 |
| | M/Mengineyo | 250,000,000.00 |
| JUMLA | | 484,242,000.00 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 943,456,000.00 |
| | M/Mengineyo | 833,200,000.00 |
| JUMLA | | 1,776,655,000.00 |
| Idara ya Utalii | Mishahara | 273,961,647.29 |
| | M/Mengineyo | 879,000,353.00 |
| JUMLA | | 1,152,962,000.29 |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | Mishahara | 1,485,826,000.00 |
| | M/Mengineyo | 650,000,000.00 |
| JUMLA | | 2,135,826,000.00 |
| **JUMLA MISHAHARA** | | **3,500,200,000.00** |
| **JUMLA MATUMIZI MENGINEO** | | **3,043,200,000.00** |
| **JUMLA KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | **6,543,400,000.00** |

**TAASISI ZA RUZUKU**

| MAELEZO | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2024- 2025 |
|---|---|---|
| | Mishahara | 1,088,170,000.00 |
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | M/Menginеyo | 375,600,000.00 |
| JUMLA | | 1,463,770,000.00 |
| **JUMLA YA MISHAHARA YA RUZUKU** | | **1,088,170,000.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **375,600,000.00** |
| **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **1,463,770,000.00** |
| | | |
| **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **4,588,370,000.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO KWA WIZARA** | | **3,418,800,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MATUMIZI YA KAWAIDA)** | | **8,007,170,000.00** |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | | |
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria | | **39,025,822,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA (MIRADI YA MAENDELEO)** | | **39,025,822,000.00** |
| **JUMLA KUU YA WIZARA** | | **47,032,992,000.00** |

**KAMISHENI YA UTALII**

| MAELEZO | MAELEZO | BAJETI YA JULAI-JUNI 2024 - 2025 |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii | Mishahara | 2,455,878,711.00 |
| | M/Mengineyo | 5,369,383,900.00 |
| JUMLA | | 7,825,262,611.00 |
| **JUMLA YA MISHAHARA** | | **2,455,878,711.00** |
| **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEO** | | **5,369,383,900.00** |
| **JUMLA KUU YA KAMISHENI YA UTALII** | | **7,825,262,611.00** |

**Kiambatisho Namba1F**

**BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 MATUMIZI | BAJETI 2024/2025 MAPATO |
|---|---|---|
| **Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale** | 32,161,649,000.00 | 900,000,000.00 |
| **Mamlaka ya Mji Mkongwe** | 10,463,770,000.00 | 289,894,000.00 |
| **JUMLA** | **42,625,419,000.00** | **1,189,894,000.00** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kuendeleza Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 MATUMIZI | BAJETI 2024/2025 MAPATO |
|---|---|---|
| **Idara ya Utalii** | 1,152,962,000.00 | - |
| **JUMLA** | **1,152,962,000.00** | - |

**Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 MATUMIZI | BAJETI 2024/2025 MAPATO |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Masoko) | 972,130,000.00 | - |
| **JUMLA** | **972,130,000.00** | **-** |

**Programu ya Kuratibu na Kusimamia Utalii**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 MATUMIZI | BAJETI 2024/2025 MAPATO |
|---|---|---|
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Mipango) | 5,607,950,611.00 | 5,000,000,000.00 |
| Kamisheni ya Utalii (Idara ya Uratibu) | 743,910,000.00 | - |
| **JUMLA** | **6,351,860,611.00** | **5,000,000,000.00** |

**Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 MATUMIZI | BAJETI 2024/2025 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | **1,776,655,000.00** | |
| **JUMLA** | **1,776,655,000.00** | **-** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamisha Mipango Mikuu ya Wizara**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 MATUMIZI | BAJETI 2024/2025 MAPATO |
|---|---|---|
| Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 484,242,000.00 | - |
| **JUMLA** | **484,242,000.00** | **-** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 MATUMIZI | BAJETI 2024/2025 MAPATO |
|---|---|---|
| Ofisi Kuu Pemba | 993,714,000.00 | 50,000,000.00 |
| **JUMLA** | **993,714,000.00** | **50,000,000.00** |

**Kiambatisho Namba1G**

**MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| TAASISI | BAJETI 2024/2025 |
|---|---|
| Mamlaka ya Mji Mkongwe | 289,894,000.00 |
| Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 900,000,000.00 |
| Ofisi Kuu Pemba | 50,000,000.00 |
| JUMLA NDOGO | 1,239,894,000.00 |
| Kamisheni ya Utalii | 5,000,000,000.00 |
| JUMLA NDOGO | 5,000,000,000.00 |
| JUMLA | 6,239,894,000.00 |

## KIAMBATISHO 2

### MPANGO WA MAFUNZO MUDA MREFU

| NA | JINA LA MTUMISHI | JINSIA | | MAFUNZO NA FANI ILIYOIDHINISHWA | CHUO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Nd. Fatma Malik Ali | | MKE | Shahada ya Kwanza ya Utawala ya Umma | Kampala University |
| 2 | Nd. Wahida Ali Khatib | | MKE | Shahada ya Kwanza Rasilimali watu | Kampala University |
| 3 | Nd. Tufah Mustafa Aboud | | MKE | Shahada ya IT | Zanzibar University |
| 5 | Nd. Maryam Mtumwa Juma | | MKE | Shahada ya Kwanza Rasilimali watu | Kampala University |
| 6 | Nd. Amina Abdulghan Othman | | MKE | Stashahada ya Rasilimali watu | ICPS |
| 7 | Nd. Ramadhan Abdalla Ameir | MME | | Shahada ya Kwanza ya Kumbukumb | IPA |
| 8 | Dawa Nyange Makame | | MKE | Shahada ya Kwanza ya Kumbukumb | IPA |
| 9 | Talhia Shamsi Ameir | | MKE | Shahada ya Kwanza Rasilimali watu | Mwalimu Nyerere |
| 10 | Muzalfat Moh'd Bakar | | MKE | Stashahada ya International Relation | IPA |
| 11 | Tatu Juma Ali | | MKE | Shahada ya Kwanza Rasilimali watu | Uganda Universtiy |
| 12 | Arafa Issa Ahmada | | MKE | Diploma in Procurement & Supply | ICPS |
| 13 | Khadija Sami Mussa | | MKE | BOA | ICPS |
| 14 | Hafidh Omar Masoud | MME | | Shahada ya Kwanza Utalii | SUZA |
| 15 | Khamis Mzee Ali | MME | | Stashahada ya Human Resource | IPA |
| 16 | Rabia Shaali Mwadini | | MKE | Shahada ya Uzamili ya Mipango | Chuo cha Mipango |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Dodoma |
| 17 | Suleiman Seif Hathar | MME | | Shahada ya Uzamili ya Mipango | OPEN UNIVERSITY |
| 18 | Abdalla Pandu Vuaa | MME | | Shahada ya Uzamili Projr | IAA |
| 19 | Said Walid Fikirini | MME | | Shahada ya Kwanza Tourism Hotel Management | Harbil University of Commerce China |
| 20 | Ahlam Othman Abdalla | | MKE | Stashahada ya Masoko na Uhusiano kwa Umma | IAA |
| 21 | Suleiman Rashida Suleiman | MME | | Shahada ya Kwanza Tourism Hotel Management | Harbil University of Commerce China |
| 22 | Ali Hamad Ali | MME | | Shahada ya Uzamivu | Ardhi University |
| 23 | Abdillahi Faki Abass | MME | | Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Umeme | Karume Institute |
| 24 | Latifa Shaibu Khamis | | MKE | Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Ujenzi | Ardhi University |